SIGNAL Publishers
Igniting thinking

# DARASA LA NANE

**SIGNAL 008**

# SIGNAL EXAMS 2021
# JARIBIO LA NANE

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.

9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.
    **Mfano**
    **Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Ujumbe mfupi unaotumwa kwa njia ya rununu huitwaje?
   A. Jarida
   B. Teleksi
   C. Ufuru
   D. Barua pepe.
   Jibu sahihi ni C. **(Ufuru)**

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

SIGNAL

*© Signal Publishers Limited 2021*

*Website: www. signalpublishers.com. Email. info@signalpublishers.com*

SignalPublishers @SignalPublishers

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Visa vya utovu wa usalama ___1___ kuongezeka ___2___ serikali kujitahidi kukabiliana ___3___. Kila uchao, kabla ya jua ___4___ magharibi, vyombo vya habari vinatufahamisha kuhusu ___5___ kwa raia au walinda usalama. ___6___ ; hali hii ___7___ mapema huenda ikaliangamiza taifa. Hatua mojawapo ___8___ kuchukuliwa ni kuwafunza polisi ___9___ bora zaidi za kukabiliana na utovu wa usalama. Aidha, raia wahimizwe kutoa mchango wao kwa ___10___ polisi kuhusu visa vyovyote vya ukiukaji wa sheria.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. unazidi | B. yanazidi | C. vinazidi | D. zinazidi |
| **2.** | A. licha ya | B. japo | C. dhidi ya | D. mithili ya |
| **3.** | A. nao | B. nayo | C. nazo | D. navyo |
| **4.** | A. kuchomoza | B. kuchwa | C. kucha | D. kukucha |
| **5.** | A. kuuawa | B. mauaji | C. kuuliwa | D. vifo |

**6.** A. Cheche ndogo hufanya moto mkubwa
B. Jahazi likipasuka kila abiria ashike ubao wake
C. Hakuna bamvua lisilo na usubi
D. Ngoma ikivuma sana hupasuka

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **7.** | A. isiyokabiliwa | B. isipokabiliwa | C. isingekabiliwa | D. isiokabiliwa |
| **8.** | A. zinazofaa | B. inaofaa | C. inayofaa | D. zinayofaa |
| **9.** | A. stadi | B. mikakati | C. hekima | D. taaluma |
| **10.** | A. vikoa vya | B. vuilinge vya | C. umati wa | D. vigaro vya |

Bi. Tatu alikuwa na mchango mkubwa wa ___11___ kwangu katika Kiswahili. ___12___ kulipenda somo hili. Aidha alinifafanulia mambo ___13___. Mathalani alinifunza matumizi mbalimbali ya kiambishi 'kwa'. Katika sentensi '___14___', kiambishi hiki kinaonyesha kusudi la kutenda jambo. Pia alinifunza matumizi ya maneno kama vile: kuliko, dhidi ya, mithili ya na kwenye ambayo yote ni ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. kuimarisha | B. kuimarika | C. kuimarishia | D. kuimarishiwa |
| **12.** | A. Alitia fora | B. Alinipiga kumbo | C. Alinitia shime | D. Alinipiga vijembe |
| **13.** | A. kadha wa kadha | B. kadhaa wa kadhaa | C. kadhaa wa kadha | D. kadha wa kadhaa |

**14.** A. Alienda kwa walimu akasaidiwe
B. Walitembea kwa maringo walipotuzwa
C. Mochama alitembelewa kwa wazazi wake
D. Tulipongezwa kwa juhudi zetu

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **15.** | A. vihusishi | B. vielezi | C. viunganishi | D. viwakilishi |

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Katika jamii ya kisasa, ushauri umechukua nafasi kubwa katika kuyarekebisha maisha ya wanajamii. Siku ambazo ilidhaniwa kuwa njia ya pekee ya kumshinikiza binadamu kuwa mwadilifu ni kupitia kwa adhabu kali zimeanza kusahaulika. Binadamu amegundua kuwa nyenzo kuu ya kumrekebisha mwenzake ni kupitia kwa kuubadili msimamo na mtazamo wa mja huyo kuhusu masuala mbalimbali. Watu ambao awali walikuwa majizi sugu wamediriki kubadili tabia zao kupitia kwa ushauri wanaopewa gerezani au katika vituo vya kubadilisha tabia.

Ushauri ni zana muhimu ya kukabiliana na visa vya utovu wa nidhamu shuleni na vyuoni. Kupitia kwa ushauri-marika ambao **umekita mizizi** shuleni na vyuoni, wanafunzi wengi ambao awali walikuwa wamedidimia katika matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vingine visivyokubalika katika jamii huweza kubadilika. Waaidha, kuna wanajamii ambao hufikwa na majanga makubwa maishani. Haya huwafanya wengine kuenda nguu. Baadhi huhiari hata kujitia kitanzi. Kupitia kwa ushauri kutoka kwa makundi na watu mbalimbali, waja hawa huonyeshwa thamani ya maisha. Baadhi yao huenda wakabadili misimamo yao kabisa na kutafuta masuluhisho kwa matatizo yao badala ya kupania kutumia njia za mkato.

Adinasi waliokabiliwa na ndwele mbalimbali huhitaji ushauri. Kuna wawele wa maradhi sugu kama vile iri na UKIMWI. Wagonjwa hawa wanapogundua kuwa wana maradhi, **huona kuwa jahazi lao limegonga mwamba**. Huandamwa na unyanyapaa wa kusikitisha. Wengine hujificha wasitake kukutana na yeyote. Hali kama hii huendelea kudhoofisha siha zao zaidi. Kupitia kwa ushauri kama vile kwenye vituo vya VCT na madaktari, wagonjwa huelekezwa kuhusu jinsi ya kuyarefusha maisha yao kwa kula lishe bora, kuwa na mtazamo chanya kuhusu maisha, kukubali hali zao na kuzichukulia kama msukumo wa kujaribu kujiendeleza badala ya kujichukulia kama wakama wa kuhurumiwa.

Mabadiliko ya nyakati, hali na hadhi humlazimu binadamu kupata mwongozo wa kuyamudu maisha yake katika hali mpya. Vijana wanapoasi ukapera na kujitoma katika asasi ya ndoa huhitaji mawaidha. Hii ndiyo sababu katika sherehe za arusi, maarusi hupewa mawaidha kuhusu jinsi ya kuishi pamoja, njia za kutatua migogoro katika ndoa na mengine mengi. Vilevile, wafanyakazi wanapokaribia kustaafu hupewa mawaidha kuhusu jinsi ya kutumia kiinuamgongo chao. Wakikosa mwongozo huenda wakatumia pesa zao vibaya na kuishia **kufutwa**.

Ushauri ni jambo muhimu maishani. Ukiwa mwanafunzi unahitaji kuelekezwa kugundua kipawa chako, kujua jinsi ya kukabiliana na masomo ambayo unayaona magumu, jinsi ya kuratibu na kutumia muda wako vyema. Aidha, unahitaji mwongozo kuhusu jinsi ya uteuzi wa marafiki na taaluma unayotaka kusomea. Bila mwongozo maisha ya binadamu huwa kama ng'ombe asiye na mchunganji. Wavyele huhitaji kuongozwa kuhusu malezi mema ya wana. Ushauri huu huweza kutolewa kupitia kwa warsha mbalimbali. Katika vikao hivi, wavyele huhamasishwa kuwa na mawasiliano na watoto wao badala ya kuwa madikteta ambao huwataka watoto wao kufuata magizo yao bila kupinga.

Kuanzia namba 16 mpaka 30, [illegible]

16. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
Mchungwa uliopandwa hapa umenawiri vizuri.
A. Michungwa yaliyopandwa hapa yamenawiri vizuri
B. Michungwa iliyopandwa hapa imenawiri vizuri
C. Michungwa uliyopanda hapa imenawiri vizuri
D. Michungwa iliyopandwa hapa imenawiri vizuri

17. Chagua orodha yenye ala za muziki pekee.
A. Tari, njuga, nyamburi.
B. Zeze, nai, baragumu
C. Msondo, baragumu, kambarau.
D. Tarumbeta, kidonywa, gitaa.

18. **Kanusha sentensi ifuatayo.**
Suruali iliyoshonwa imemtoshea mtoto.
A. Suruali isiyoshonwa haikumtoshea mtoto.
B. Suruali iliyoshonwa haimtoshei mtoto.
C. Suruali iliyoshonwa haijamtoshea mtoto.
D. Suruali iliyoshonwa haikumtoshea mtoto.

19. Ni sayari ipi ina joto kuliko zote?
A. Zuhura B. Zaibaki.
C. Mirihi D. Mshtarii.

20. **Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi ifuatayo.**
Naenda kwa bibi kumchanjia kuni.
A. Kuonyesha kihusishi
B. Kuonyesha nafsi
C. Kuonyesha kuendelea kwa kitendo
D. Kuonyesha umilikaji.

21. **'Shinda'** ni kuwa wa kwanza katika jambo. **'Shinda'** pia ni
A. bila kujaa
B. tatizo
C. kutoweza jambo
D. kukesha mahali.

22. **Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo.**
Mwizi aliiba kikapu chenye ndizi.
A. Majizi waliiba majikapu yenye madizi.
B. Jimwizi liliiba jikapu lenye dizi.
C. Jizi liliiba kapu lenye madizi.
D. Jizi aliiba jikapu lenye dizi.

23. **Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kuamrisha.**
A. Lo! Mbona unamchelewesha mtoto mdogo mzito
B. Mungu alifanya bidii akafaulu
C. Ukimweleza hoja yako atakuelewa
D. Someni magazeti ya Kiswahili mara nyingi

24. Ni msemo gani ulio na maana ya kutembea mwendo mrefu kwa miguu?
A. Piga mihundi
B. Piga mlazamlaza
C. Enda pesha
D. Enda tete

25. Kutokana na kitenzi **samehe**, tunaunda kivumishi
A. msamaha
B. sameheyu
C. kusamehe
D. samehewa.

26. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Ale asile tumbo lake limejaa.
A. Fisi.
B. Nondo.
C. Sahani.
D. Mtungi.

27. Neno **'mbwakoko'** lina silabi ngapi?
A. Tatu
B. Mbili
C. Nne
D. Nane.

28. Buibui ni kwa utando kama ilivyo kasuku kwa
A. kizimba
B. tundu
C. kiota
D. pango.

29. **Badili sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.**
Juma: Nitakujibia swali hilo kesho.
A. Juma aliambiwa kuwa atajibiwa swali hilo siku ambayo ingefuata.
B. Juma alimwambia kuwa angemjibia swali hilo siku ambayo ingefuata.
C. Juma amemwahidi kwamba atamjibia swali hilo kesho.
D. Juma alimwahidi kwamba angemjibia swali hilo kesho.

30. Methali gani hailingani na nyinginezo?
A. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
B. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.
C. Dunia ni msumeno hukata mbele na nyuma.
D. Aliye juu mngoje chini.

31. Ni kweli kusema kwamba
A. adhabu haimfanyi mtu kuwa mwadilifu
B. watu waliopitia adhabu kalikali huwa waadilifu kuliko wenzao
C. wakati mwingine adhabu haileti matokeo mazuri kama nasaha
D. ushauri ulitumiwa tangu zamani kurekebisha tabia badala ya adhabu.

32. Aya ya kwanza imebainisha kuwa
A. mtu akihimizwa kubadili mtazamo huweza kuwa na mienendo ifaayo
B. ushauri ufaao hupatikana wanakotengewa watu kwa adhabu
C. kutumwa kwenye vituo vya kurekebishia tabia huwafanya wengi kubadilika
D. ni vizuri kuwashauri wahalifu badala ya kuwafungia gerezani.

33. Nahau **'umekita mizizi'** ina maana gani jinsi ilivyotumika?
A. Umezidi kuzorota.
B. Umeimarika zaidi.
C. Unasifika sana.
D. Unaendelea kudidimia.

34. Matokeo ya ushauri nasaha wa marika shuleni ni yapi kulingana na kifungu?
A. Kuangazia matumizi mabaya ya dawa.
B. Kuwakashifu wanaotumia dawa za kulevya.
C. Uhusiano mwema baina ya waraibu na wenzao.
D. Kukatizwa kwa uraibu usiokubalika.

35. Msimamo wa mwandishi wa makala haya ni kuwa
A. kutopata ushauri ufaao kunaweza kumfanya mtu kuchukua hatua zisizofaa
B. waja wengi wanaokabiliwa na majanga huishia kujitia kitanzi
C. idadi kubwa ya vifo hutokana na kutoelewa thamani ya maisha
D. kwa kawaida vijana ndio wanaotatuhisha matatizo yao kwa njia za mkato.

36. Maana ya kifungu **'huona kuwa jahazi lao la maisha limegonga mwamba'** ni
A. kuhisi kuwa wanapuuzwa na wenzao
B. kuona kuwa maisha yao yameanza kubadilika
C. kutokuwa na matumaini ya kuishi
D. kutojua umuhimu wa maisha ya wenzao.

37. Kinachowadhoofisha zaidi watu wenye magonjwa sugu ni
A. makali ya maradhi hayo
B. unyanyapaa katika jamii
C. kunyimwa dawa wanazohitaji
D. kuwekwa peke yao hospitalini.

38. Mwanafunzi hushauriwa kwa yote haya ila
A. kuutambua uwezo wake ili kujiendeleza
B. namna ya kuratibu muda wake ipasavyo
C. kuwa na mahusiano yanayofaa
D. jinsi ya kuvitambua vipaji vya wenzake.

39. Kulingana na aya ya mwisho
A. ni vyema watoto wafuate maagizo ya wazazi bila kupinga
B. panapo maelewano matokeo ya malezi bora huafikiwa
C. watoto hufunzwa malezi bora kupitia warsha mbalimbali
D. vijana hawapendi kutii kwa kuwa wanajua wazazi ni madikteta.

40. Neno **kufutwa** kulingana na kifungu lina maana ya
A. kuachishwa kazi
B. kufuja mali
C. kupoteza mali
D. kushindwa na jambo.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Naikumbuka siku hiyo ya Jumamosi vizuri sana. Msena wangu wa kufa kuzikana alimzuru kwetu na kumpata mimi na mnuna wangu tukipalilia mihogo shambani. Wavyele wetu walikuwa wameenda sokoni kuchuuza mboga na nafaka ili wayakidhi mahitaji yetu. Baada ya kutuamkia, Boru alielekea kwenye stoo yetu akachukua jembe na kufululiza moja kwa moja hadi pale tulipokuwa. Alitusaidia kuipalilia mihogo ile na kufumba na kufumbua tukawa tumeikamilisha gange ile. Ama kweli, bandu bandu humaliza gogo.

Baada ya kazi tulirejea nyumbani tukaandaa kishuka na kushtaki njaa. Hapo ndipo Boru alipopendekeza tuelekee kwenye Mto Thiba tukapige kachombe. Mto huu ulitisha sana sio tu kwa mkondo wake wa kasi na maji ya kina kirefu bali pia uwepo wa wanyama hatari kama vile mamba na viboko. Wavyele wangu walinitahadharisha mara nyingi dhidi ya kuenda kuogelea mtoni humo. Japo haikuwa mara ya kwanza kwangu kuukaidi waadhi huu, nilishindwa kuelewa ni kwa nini niliingiwa na wayowayo kiasi. Hata hivyo, hamu ya kujiburudisha majini na ile hali ya kutotaka kumvunja moyo somo yangu ilinifanya kupuuza hisia hizi.

Tulipowasili kwenye ukingo wa mto, tulizivua lebasi zetu na kupiga mbizi kwa ustadi. Wakati mwingine tulijizamisha hata kwa zaidi ya dakika nzima ili kudhihirisha ustadi wetu. Mara nilihisi mguu wangu ukibururwa ndani ya maji. Nilidhani kuwa Boru au mnuna wangu alikuwa akinichezea shere. Niliendelea kucheka huku nikijizatiti kujinasua. Nilipoangalia kando na kuwaona wakiogelea mbali kidogo, hofu ilinivamia ghafla na kunivaa mzimamzima. Wakati uo huo, nikahisi maumivu makali mguuni pangu.

Masalale! Kumbe mamba alikuwa akijaribu kuniburura akinielekeza kwenye maji marefu. **<u>Nilipiga usiahi ambao ungetetemesha hata mlima</u>**. Boru alipoyaona haya, alizichukua nguo zake na kuparakasa mbio za visigino kushikana na kisogo. Mnuna wangu naye, licha ya udogo wake, alichukua kipande cha tawi la mti na kuanza kumhujumu hayawani yule. Awali, kiumbe yule alizidhihaki juhudi zetu zote lakini baadaye akaanza kusalimu amri. Meno yake yaliuachilia mguu wangu uliosheheni majeraha makubwa.

Kule chengoni, wavyele wetu walitusaka kwa majirani wakatukosa. Ghafla msako wa kututafuta ukaanzishwa. Wazazi na majirani walijigawa katika makundi, wengine wakaelekea msituni, kwenye mashamba ya matunda na viazi vitamu huku wengine wakija upande wa mtoni. Kundi hili lilipowasili, lilipata ndipo mnuna wangu anaponiokoa kutoka kwenye hatari ile. Walinitoa wakanilaza kando na kunifanyia huduma ya kwanza. Wengine walimfuatilia hayawani yule na kumwangamiza.

Baada ya kupewa huduma ya kwanza, jirani mmoja aliiendea baiskeli yake na kusaidia kunifikisha hospitalini. Nililazwa kwa muda mrefu nikiwa si hayati si mamati. Mungu hawachi mja wake. Hatimaye nilianza kupata nafuu. **<u>Tangu siku hiyo, maneno ya wavyele wangu yalianza kuwa na maana kwangu.</u>** Aidha, uhusiano wangu na Boru umegeuka kuwa baridibaridi. Japo anaweza kujitetea kwa kusema kuwa kunguru mwoga hukimbiza ubawa wake, kwangu mimi huyo ni mla nawe ambaye hafi nawe.

41. Kulingana na aya ya kwanza
A. msimulizi na ndugu yake mkubwa walikuwa wakipalilia mimea shambani
B. familia ya msimulizi ilishiriki kilimo na biashara
C. wazazi walimwachia msimulizi na nduguye kazi nyingi kabla ya kuondoka
D. shamba la familia ya msimulizi lilipandwa mihogo pekee.

42. Yawezekana Boru alizoea kuenda kwa akina msimulizi kwani
A. alijitolea kuwasaidia katika kazi zao
B. alifika hadi shambani kuwajulia hali
C. alielewa vizuri kuwa wazazi wameondoka
D. alijua mahali pa kulipata jembe la kulima.

43. Kulingana na kifungu hiki, Mto Thiba ulikuwa wenye
A. maji mengi na unaoogopwa na wote
B. wanyama hatari na maporomoko ya kutisha
C. maji yaendayo kasi na wanyama wanaotisha
D. maji ya kina kirefu na kila aina ya wanyama.

44. Msimulizi anasema kwamba
A. haikuwa mara ya kwanza kukiuka maagizo ya wazazi
B. hakuzoea kuenda kuogelea mtoni
C. kuwazia hatari ya mto kulimtia wasiwasi
D. wazazi walijua kuwa alizoea kuogelea mtoni.

45. Kwa nini hasa msimulizi alikubali kuenda kuogelea?
A. Alishawishiwa na rafikiye na ndugu yake.
B. Alichelea kumkasirisha rafiki yake.
C. Alizoea kusikia watu wakisifu uogeleaji.
D. Alijua kuwa maji ya Mto Thiba yaliburudisha.

46. Mwandishi alijuaje kuwa aliyemvuta hakuwa rafikiye wala nduguye?
A. Aliwasikia wakipiga unyende kwa mbali.
B. Alihisi maumivu makali mguuni.
C. Aliwaona wakiogelea mbali na pale alipokuwa.
D. Alitarajia kusikia vicheko vya wenzake.

47. Sentensi **'nilipiga usiahi ambao ungetetemesha hata mlima'** imetumia tamathali gani ya semi?
A. Tashbihi.
B. Tashhisi.
C. Kinaya.
D. Chuku.

48. Ni methali gani inayoafikiana vizuri na aya ya nne?
A. Zimwi likujualo halikuli likakwisha.
B. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
C. Kikulacho ki nguoni mwako.
D. Damu ni nzito kuliko maji.

49. Ni wazi kuwa jamii ya msimulizi
A. ni yenye mapuuza
B. inathamini ushirikiano
C. ni wacha Mungu
D. ina watu jasiri sana.

50. Maneno yaliyoangaziwa katika aya ya mwisho yanaashiria kuwa
A. awali, msimulizi alipuuza ushari wa wazazi
B. siku zote, msimulizi alithamini mawaidha ya wazazi
C. mwandishi anayaona waziwazi aliyoambiwa kuhusu Boru
D. awali, msimulizi hakujua umuhimu wa uhusiano mwema.

***TANBIHI:** Ili kudurusu kwa kina katika somo la Kiswahili, jipatie nakala ya 'KICHOCHEO CHA KISWAHILI' kutoka Signal Publishers. Kinapatikana katika maduka ya vitabu kote nchini.*